# ILANI YA UCHAGUZI MKUU WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI

CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO

CHADEMA



*Ni Wakati wa Mabadiliko*

*Kuondoa Umaskini Chagua CHADEMA*

**Oktoba, 2015**


'KUWA CHACHU YA MABADILIKO
UNAYOTAKA KUYAONA'

# ILANI YA UCHAGUZI MKUU WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI

CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO

CHADEMA



*Ni Wakati wa Mabadiliko*

*Kuondoa Umaskini Chagua CHADEMA*

**Oktoba 25, 2015**

# YALIYOMO


Salaam za Mwenyekiti........................................................ V

Salaam za Wagombea........................................................ Vii

Utangulizi........................................................................ 1

Falsafa na Misingi ya Sera na Itikadi ya Siasa za CHADEMA.. 4

Katiba ya Wananchi na Mabadiliko Makubwa ya Mfumo wa Utendaji na Uwajibikaji wa Serikali na Kurudisha Uzalendo........................................................ 8

Elimu Bora Kwa Watanzania Wote.................................. 17

Afya na Hifadhi ya Jamii.................................................. 23

Ardhi, Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi.................................. 29

Miundombinu: Reli, Bandari, Barabara, Usafiri wa Anga na Usafiri wa Majini.............................................. 37

Viwanda........................................................................ 43

Uchumi Shirikishi, Biashara, Fedha na Mitaji.................... 47

Nishati, Madini, Gesi na Mafuta........................................ 53

Maliasili na Utalii.............................................................. 61

Ajira, Vijana na Wanawake.............................................. 65

Sanaa, Utamaduni na Michezo........................................ 70

Ulinzi, Usalama na Haki za Raia........................................ 74

Sera ya Mambo ya Nje Yenye Tija.................................. 79

# Salaam za Mwenyekiti

***Ndugu Mtanzania mwenzangu***



Karibu usome ilani hii ya CHADEMA iliyo na mtazamo wa pamoja wa vyama shirika vya Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ambavyo ni NLD, NCCR-Mageuzi, CUF na CHADEMA.

UKAWA inajengwa katika msingi mkuu wa kubadilisha katiba iliyopo ili kuweka katiba ya wananchi kwa ajili ya maendeleo yao. Katika kipindi hiki ambacho hali ya maisha ya Watanzania imeendelea kuwa duni, uchumi wa nchi yetu umeyumba, ubora wa elimu ni wa mashaka, ajira kwa vijana ni za kubahatisha na ukiukwaji na uvunjifu wa haki za binadamu umekithiri; uongozi thabiti wenye uadilifu na uzalendo unahitajika kuivusha nchi yetu ili tufike salama.

UKAWA kupitia CHADEMA ikiingia madarakani imedhamiria kubadilisha maisha ya mtanzania mmoja mmoja na kuboresha maisha ya watanzania wote kwa ujumla kwa kuondoa umaskini, kudumisha amani na kuhimiza uzalendo na uwajibikaji, kuimarisha umoja na Muungano wetu. **Nawaomba watanzania wenzangu wote muisome ilani hii, kuijadili na kuitafakari ili muweze kufanya maamuzi sahihi katika mwaka huu wa mabadiliko.**

Mh. Freeman Aikael Mbowe
**Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa**


CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO
CHADEMA
TBC

# Salaam za Wagombea

## MGOMBEA URAIS JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Mimi **Edward Ngoyai Lowassa**, mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ndugu Watanzania wenzangu

Kupitia uchaguzi mkuu ujao, Watanzania tuna fursa ya pekee kuuondoa utawala wa CCM madarakani na kuleta mabadiliko ya kweli nchini.

Ilani hii ni dira ya maendeleo na kuondoa umaskini itakayosimamiwa na CHADEMA na ushirika wa UKAWA. Azma hii haiwezi kuhitimika bila ushiriki wa kila Mtanzania anayependa maendeleo na kuitakia nchi yetu heri kuniunga mkono mimi, mgombea mwenza, mgombea wa Urais Zanzibar, wabunge/ wawakilishi na madiwani kupitia UKAWA.

Tafadhali isome ilani hii kwa makini, itafakari na ujiridhishe kuwa inalenga kuivusha Tanzania kutoka mashaka, unyonge, umaskini na kukata tamaa kwa wananchi kuliko sababishwa na mfumo mbovu wa kiutalawa uliojaa rushwa na ufisadi kwenda kwenye serikali itakayojengwa na mfumo wa utawala bora wenye kupelekea kuwa na Taifa lenye neema, matumaini na maendeleo ya kweli.

**Pamoja Tutashinda**



***"KUWA CHACHU YA MABADILIKO UNAYOTAKA KUYAONA"***

# Salaam za Wagombea

## MGOMBEA MWENZA URAIS JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Mimi **Juma Duni Haji**, mgombea mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania


Ndugu zangu Watanzania

Zaidi ya miaka hamsini ya Uhuru na Muungano wa Zanzibar na Tanganyika bado nchi yetu inakabiliwa na matatizo ya kimsingi ikiwemo rushwa na ufisadi.

Elimu, mfumo wa afya na miuondombinu duni, umaskini, ukiukwaji wa haki bado ni sehemu kubwa ya maisha ya Watanzania. Kupitia ilani hii, CHADEMA na UKAWA tunalenga kumkomboa kila mwananchi kutokana na hali kandamizi ya utawala wa CCM, kuondoa umaskini, kuleta maendeleo na kusimamia haki na usawa.

Vilevile tutaimarisha udugu na ushirikiano wa pande zote za Muungano kwa misingi ya haki na usawa. Tafadhali soma ilani hii, itafakari na ujiridhishe kuwa ni dira ya uhakika ya kuivusha Tanzania katika safari yakuelekea maendeleo na neema nchini.

**Pamoja Tutashinda**



# UTANGULIZI

Historia inaonyesha kuwa Vyama vikongwe Barani Afrika vimeanguka kutokana na sababu mbalimbali hasa kukithiri kwa umasikini na ukosefu wa ajira; ajira za upendeleo; kukua kwa matabaka hasimu kwenye jamii; rushwa, ufisadi, ubadhirifu na matumizi ya anasa serikalini.

CHADEMA inatambua sababu kuu nne zilizosabisha nchi yetu ifike katika umaskini uliokithiri wakati inazo rasilimali za kutosha. Sababu hizo ni:

1. Ukosefu wa katiba ya wananchi ambayo ingewapa mamlaka ya kuwadhibiti watawala.
2. Ukosefu wa uongozi wenye uzalendo, uadilifu na utawala bora ambao umepelekea uzembe na kutowajibika; na kukithiri kwa ufisadi na ubadhirifu wa mali ya umma.
3. Kufanya uchumi utumikie siasa badala ya siasa kutumikia uchumi – kupuuza ushauri wa kitaalamu katika sera, mipango na utekelezaji.
4. Ukiritimba wa Madaraka wa Chama kimoja.

Viashiria vinaonyesha kwa kiasi kikubwa kuwa tayari serikali ya CCM ni dola inayoanguka. CHADEMA na UKAWA wanadhamiria kuunda serikali itakayoondoa mambo yote hayo ili kujenga upya Taifa imara kwa manufaa ya Watanzania wote.

Lengo kuu kwa ujumla katika ilani hii, ni kuhuisha uzalendo, uadilifu na uwajibikaji katika uongozi wa nchi ambao ndio msingi mama wa kuleta maendeleo ya jamii ya Watanzania. Ili tuweze kutoka hapa tulipo tunahitaji uongozi utakaozingatia

yafuatayo ambayo ndiyo msingi wa ilani hii:

- Kuimarisha amani, umoja na mshikamano wa Taifa
- Kuleta Katiba ya Wananchi inayosimamia haki na usawa
- Kujenga Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa misingi ya usawa
- Kuleta fikra ya Watanzania kujiamini na kujitegemea kama Taifa huru
- Kuimarisha Uzalendo na Uadilifu
- Kujenga Uchumi shirikishi unaolenga kuondoa umaskini
- Kuimarisha Huduma za Jamii
- Kuwajengea mazingira mazuri na kuwapa kipaumbele Walemavu katika sekta zote
- Kujenga Utendaji bora na Uwajibikaji katika sekta ya Umma
- Kujenga Ushirikiano wa karibu baina ya Serikali na sekta binafsi
- Kudumisha na kuendeleza uhuru wa mawazo, uhuru wa kutoa na kupata habari na kujumuika na watu wengine
- Ulinzi thabiti na usalama wa raia.
- Ushirikiano wa Kimataifa wenye tija na Ujirani mwema.

Ni dhamira ya CHADEMA na UKAWA kuunda serikali makini, adilifu na inayowajibika kwa umma, katika kuendeleza falsafa ya CHADEMA msingi wa juhudi zote za maendeleo za uchumi na kijamii zitalenga kwenye kuondoa umaskini na kuelekea kwenye taifa la uchumi wa kati na hatimaye lililoendelea. Vipaumbele wa mwelekeo huo ni kama ilivyoelezwa kwenye sura zinazofuata kwenye ilani hii.

## Wakati na Fursa ya Kufanya Mabadilikoni ni Sasa

Ilani hii inaainisha maeneo na vipaumbele vitakavyozingatiwa na CHADEMA na UKAWA mara watakapopata fursa ya kuunda serikali. Serikali mpya ya UKAWA inalenga katika kujenga uchumi imara na shirikishi na kuunda serikali ndogo yenye kuzingatia uadilifu, ufanisi, tija, uzalendo, uwajibikaji na nidhamu katika matumizi ya rasilimali za nchi. Serikali itabadili mfumo wa utawala uliopo kutoka utawala kandamizi, kwenda utawala unaoheshimu wananchi na matakwa yao. Ilani hii sio ahadi bali ni Dira ya Taifa letu chini ya serikali ya CHADEMA/ UKAWA na inayotekelezeka.

Kwa ufupi, Ilani hii inabeba maono na mwelekeo wa CHADEMA na vyama vinavyounda UKAWA kwa lengo la kuomba ridhaa ya wananchi ili kuanza ujenzi mpya wa Taifa letu kwa kipindi cha miaka Mitano (2015-2020).

Ndugu Mtanzania,

Safari ya Mabadiliko ya kweli inaanza sasa. Ungana na CHADEMA/UKAWA uwe sehemu ya mabadiliko haya ambayo Watanzania wameyatafuta kwa muda mrefu. Tumia fursa hii adhimu uliyonayo ya uchaguzi kufanya mabadiliko.

**Kuondoa Umasikini, Chagua CHADEMA/UKAWA.**

- **Mchague Mh. Edward Ngoyai Lowassa -Rais**
- **Mchague Mh. Juma Duni Haji- Makamu wa Rais**
- **Chagua Wabunge/Wawakilishi kutoka UKAWA**
- **Chagua Madiwani kutoka UKAWA**

# FALSAFA NA MISINGI YA SERA NA ITIKADI YA SIASA ZA CHADEMA

Misingi ya ilani CHADEMA imejengwa juu ya falasafa ya NGUVU NA MAMLAKA YA UMMA na itikadi ya MLENGO WA KATI; na ni kama ifuatavyo:

**Misingi itokanayo na Falsafa:**

- Umma ndiyo wenye madaraka ya mwanzo na mwisho kuhusu hatima ya nchi.
- Nguvu na Mamlaka ya Umma vitajenga na kudumisha Demokrasia kuendana na katiba.
- Nguvu na Mamlaka ya Umma ndiyo msingi wa kuhoji na kuwajibisha uongozi uliochaguliwa kwa uhuru na kwa haki.
- Nguvu na Mamlaka ya Umma ndiyo chombo cha kuwaamsha, kuwahamasisha, na kuwaelimisha Watanzania waimiliki, waitawale, wailinde, waiendeshe na waiendeleze nchi kwa ubunifu ili wanufaike nayo.

**Misingi itokanayo na Itikadi:**

- Kukuza na kuimarisha uchumi wa soko huru lisilokuwa holela, kupitia rasilimali ili umma unufaike.
- Kuthamini umuhimu wa familia, uzalendo na mila na desturi zilizo nzuri.
- Kusimamia zaidi maslahi ya Taifa kuliko ya vyama vya siasa.
- Kujenga uwiano bora kati ya maslahi binafsi na maslahi ya umma.
- Uhuru wa kuabudu bila kuingiliana na dola.
- Kuwajengea uwezo wananchi kumiliki na kuendesha uchumi.

- Kila mtu kutimiza malengo yake na kufanikiwa kadiri ya vipaji vyake.

**Kuleta Mabadiliko**

Ili tuweze kuleta mabadiliko ya kweli katika uchaguzi huu wa mwaka 2015, kuna mambo mawili ya msingi ya kuzingatia.

- Ni muhimu tuelewe na tuwe wakweli juu ya chanzo cha matatizo yetu na ni kwa namna gani tumefika hapa tulipo leo. CHADEMA/UKAWA tunaamini kwa dhati kuwa tatizo mama lililotufikisha hapa tulipo ni udhaifu wa kimuundo, kiutendaji na kiuongozi uliojengwa na Chama Cha Mapinduzi kwa zaidi ya miaka 50. CHADEMA/UKAWA tutajenga Taifa letu kwa kufanya mabadiliko makubwa na ya haraka ya kiutendaji, kimuundo na kiuongozi ili kurudisha uwajibikaji katika ngazi zote za utawala wa nchi. Hili ndilo litakuwa lengo kuu la utendaji wa Serikali itakayoundwa baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2015.
- Watanzania tutambue kwamba tukiamua kwa dhati na kuchukua hatua katika uchaguzi huu wa Oktoba 2015 tuna uwezo wa kubadili hali ya kiuchumi na kijamii tuliyo nayo kutoka taifa lenye uchumi mdogo kabisa duniani na kuwa taifa lenye uchumi wa kati na hatimaye taifa lililoendelea kiuchumi na kijamii. Uchaguzi huu ni nyenzo muhimu na ya pekee ya kuweza kubadili hali ya nchi yetu na kurudisha matumaini kwa Watanzania wote bila kujali hali, itikadi, rangi, kabila, dini au kitu kingine chochote ambacho kinaweza kumtofautisha Mtanzania mmoja mmoja au kwa makundi mbalimbali.

**Maadili na uadilifu**

- Tanzania ni nchi yenye historia iliyoundwa na maadili, uadilifu na uzalendo. Waasisi wa Taifa hili walikuwa na ndoto ya Tanzania ambayo ingejengwa katika misingi hiyo.
- Ni matumaini ya CHADEMA/UKAWA kwamba mabadiliko ambayo wananchi wameamua kuyafanya juu ya uongozi wa nchi yao yanarejesha maadili, uadilifu, uzalendo pamoja na nidhamu katika uongozi wa nchi na watanzania kwa ujumla.
- CHADEMA/UKAWA wana jibu la ndoto za watanzania. Ni dhahiri na ni kweli kwamba tumekosea njia kama Taifa, hivyo ni sisi wananchi tunaotakiwa kujikosoa, kubadili njia potofu na kurudi katika misingi sahihi ili kuhakikisha kwamba tunakuza usawa kati ya watu wetu chini ya utawala ya sheria na viongozi wanaoongoza kwa mfano. **Tumia kura yako kwa usahihi ili uweze kusahihisha makosa yaliyokwisha tokea kwa kuchagua CHADEMA/UKAWA**.
- CHADEMA/UKAWA tunaamini kwamba tunahitaji kurudi katika misingi hiyo upya na tunaona fahari kubwa kuitangaza na kuisimamia kwa niaba ya watanzania wote. Falsafa yetu ni nguvu ya umma na Umma ndio wenye mamlaka ya mwisho katika mustakabali wa Taifa kwani ndiyo wenye mamlaka ya kuweka viongozi madarakani na kuwawajibisha kiutendaji pale watakavyofanya kinyume na matarajio yao.



# KATIBA YA WANANCHI NA MABADILIKO MAKUBWA YA MFUMO WA UTENDAJI NA UWAJIBIKAJI WA SERIKALI NA KURUDISHA UZALENDO



**Hali halisi**

<u>*Katiba ya wananchi*</u>

- Kutokuwa na katiba bora kumewanyima Watanzania mamlaka ya kuwajibisha viongozi wao, kukosekana kwa dira, tunu za Taifa, maadili na miiko ya uongozi; na kukosa Muungano ulio imara kimuundo.
- Pia kukosekana kwa katiba ya wananchi kumepelekea mfumo wa serikali kiutendaji kuwa mbovu kwani hakuna vyombo huru kama Taasisi ya kupambana na rushwa, ofisi ya mkaguzi mkuu wa serikali, mahakama na vyombo vya dola.
- Kutokuwepo kwa ugatuzi wa kweli wa mamlaka ya serikali kuu kwenda karibu na wananchi kumepelekea

watanzania kutoshiriki katika maamuzi ya vipaumbele vyao na kutoshirikishwa katika kupanga na kuisimamia bajeti za maendeleo yao kikamifu na hivyo kuzorotesha maendeleo.




*Utendaji na Uwajibikaji*

- Pamoja na uwepo wa sheria na miongozo thabiti ya utumishi wa umma, poromoko kubwa la maadili katika uongozi na jamii kwa ujumla limepelekea watumishi wachache kutimiza wajibu wao kwa ufanisi na kwa muda stahiki huku kukiwepo na ongezeko kubwa la uzembe, rushwa, wizi na ufisadi wa mali ya umma miongoni mwa viongozi wa kisiasa na watumishi wa umma. Hii inachangia rasilimali kubwa ya nchi kutonufaisha wananchi wengi badala yake wachache hasa walio kwenye madaraka. Vile vile ukosefu wa umakini, nidhamu, ubunifu na uthubutu katika utendaji

kazi kumesababisha utendaji mbovu wa serikali na kutowajibika kwa watumishi wa umma. Sababu hizi kwa pamoja kwa kiasi kikubwa kumechangia kudorola kwa uchumi wa Taifa letu.

- Kutokokuwepo kwa uhuru wa vyombo vya habari na hivyo kupelekea kutoibua na kuwajuza wananchi maovu ya serikali ikiwemo rushwa na ufisadi.

- Watumishi hasa sekta ya umma kutohamasika kufanya kazi kwa bidii kunatokana na maslahi duni na mishahara isiyo na uhalisia na hali ya maisha kwenda na ujuzi, nafasi na vyeo kazini.

**Fursa iliyopo**

- UKAWA iliyoanzishwa kutetea katiba ya wananchi ilisusia bunge la katiba lililokuwa chini ya wingi wa CCM ambalo lilitupa maoni ya wananchi. Sasa umoja huu umeimarika na sasa unaingia katika uchaguzi ukiwa kitu kimoja na lengo kuu likiwa ni kushinda uchaguzi ili kuwaletea Watanzania katiba bora. Upinzani unaunganishwa na kutaka kupitishwa katiba mpya ya mabadiliko ya jinsi tunavyoongozana kama vile kuwa na muundo wa serikali tatu yaani serikali ya Zanzibar, serikali ya Tanganyika na Serikali ya Muungano yenye usawa ambayo itaimarisha muungano, bunge na baraza dogo la mawaziri la serikali ya Muungano.

- Uimara wa upinzani wa kusimamia hoja za kitaifa bungeni na nje ya bunge unatoa fursa kwa UKAWA kuunda serikali itakayosimamia sheria na miongozo ya

serikali yenye kufuata haki kwa kila mtanzania ili kuleta mabadiliko makubwa katika utendaji wa serikali na wananchi kwa ujumla.

**CHADEMA itafanya nini**

- Katiba ya wananchi ni kipaumbele namba moja, hivyo serikali ya CHADEMA itaanzisha tena mchakato wa katiba uliozingatia maoni ya wananchi. Lengo ni kuhakikisha kwamba vifungu vinavyohusu tunu, maadili na miiko ya uongozi vinakuwa kwenye katiba mpya ili sheria na kanuni mpya ziweze kutungwa na kudhibitiwa
- Kujenga uzalendo ili kila Mtanzania aweze kutathmini mchango wake kwa taifa kila siku
- Kuimarisha nidhamu, utendaji na uwajibikaji katika Sekta ya Umma
- Kuimarisha mchango wa Wataalam katika uendeshaji wa nchi
- Kusimamia ukusanyaji na matumizi mazuri ya kodi na mapato ya serikali na kupunguza mzigo wa kodi kwa wananchi
- Kuboresha maslahi na vitendea kazi kwa watumishi wa Umma
    - *Ikiwa ni pamoja na kupunguza kodi kwa wafanyakazi ili kupunguza ukali wa maisha*
    - *Kwa mtumishi atakayependa, atalipwa mshahara wa mwezi kwa awamu mbili katika mwezi ili kwendana na uhalisia wa hali ya maisha na kupunguza kukopa kopa kusiko kwa lazima*
- Kudhibiti na kupunguza matumizi ya serikali ikiwa ni pamoja na kufuta safari za watumishi serikalini zisizokuwa

muhimu pamoja na zile za Rais na kupiga marufuku matumizi ya magari ya anasa serikalini (mashangingi)

- Kudhibiti deni la Taifa kwa kuanza na ukaguzi wa madeni ya serikali ili kuhakiki jinsi yalivyotumika
- Kuimarisha uwazi na kuondoa usiri katika shughuli za serikali na kuweka bayana mikataba yote ya nchi ikiwa ni pamoja na ile ya mafuta, madini na gesi asilia ili watanzania waweze kuihakiki na Bunge lao liikubali kabla ya kupitishwa na serikali
- Kuzingatia na kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari kwa kuhakikisha kwamba tunafuta sheria zote ambazo zinaingilia uhuru wa vyombo hivyo
- Kuimarisha serikali za mitaa ili wananchi washiriki kikamilifu katika maendeleo yao.

*Vita dhidi ya rushwa na ufisadi*

- Katika matatizo yote yanayoikabili Taifa letu moja wapo ambalo linagusa kila Mtanzania kila sehemu ya maendeleo ya uchumi na jamii ni tatizo la rushwa na ufisadi. Tatizo hili limekua sugu katika nchi yetu na CCM kwa miaka mingi imeahidi kupambana nalo bila mafanikio.
- Akizungumza na Radio ya Umoja wa Mataifa mnamo tarehe 9/12/2014, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alisema tatizo la rushwa linasababishwa na udhaifu wa serikali kutotekeleza mapendekezo ya ripoti ya CAG na pia udhaifu wa Serikali katika kuwachukulia hatua wabadhilifu. Pia alisema tatizo linatokana na siasa ya kijasiliamali "entrepreneurial politics" ambapo

viongozi wanafanya maamuzi kwenye mambo ambayo wana maslahi binafsi. Alitolea mfano wa rushwa mbaya kabisa Tanzania ambapo viongozi wa serikali waligawana nyumba za serikali ambazo zimejengwa kwa kodi ya Watanzania wote. Katika kutokomeza kabisa tatizo la rushwa na ufisadi, CHADEMA/UKAWA tutaanzisha vita ya kisayansi.

- CHADEMA inaamini kwamba maendeleo ya kweli ya Tanzania yataletwa tu na Serikali itakayokuwa na nia na mikakati ya ukweli wa kupambana na kuondoa rushwa na ufisadi siyo kwa maneno kama ilivyozoeleka lakini pia kwa vitendo. Katika hili lazima ieleweke kwamba rushwa siyo kwamba iko sekta ya umma pekee yake bali inaunganisha sekta za umma na sekta za binafsi ambako ndio fedha kubwa ya rushwa zinakotoka. Ni pale tu mafanikio ya kupambana na rushwa na ufisadi yatakapoanza kutekelezwa kwa dhati kwamba mabadiliko makubwa na maendeleo katika sekta mbalimbali zilizotajwa katika Ilani hii.
- CHADEMA itaratibu kuwepo kwa mustakabali mpya wa sekta binafsi kutimiza wajibu wake katika kupambana na rushwa na ufisadi.
- CHADEMA itaendeleza utashi wake wa kisiasa ili kuhakikisha kwamba vita dhidi ya rushwa na ufisadi inatekelezwa kwa sawia bila woga, kulindana, upendeleo au chuki binafsi.
- Swala la maadili ya viongozi na watendaji wa Umma litawekwa kwenye katiba na kuanzisha chombo huru na imara cha kusimamia maadili ya viongozi na watendaji serikalini.

- Kutekeleza kwa ukamilifu ripoti za CAG na hasa kuwachukulia hatua wabadhirifu walioainishwa kwenye ripoti zake.
- Kuimarisha na kutumia sheria na vyombo viliopo kama Economic and Organised Crime Act na PCCB Act na vyombo vya sheria kama PCCB, Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka na Mahakama kuhakikisha kwamba wanaohusika na rushwa na ufisadi wanachukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na vifungo vya muda mrefu na kurejeshwa kwa fedha walizowaibiwa Watanzania ziwe ndani au nje ya nchi.
- Kubadilisha mfumo ili chombo chenye mamlaka katika kusimamia sheria ya rushwa na ufisadi yaani Takukuru kinakuwa ni chombo huru kinachotambuliwa na Katiba na kuwajibika moja kwa moja kwa Bunge.
- Kuwaongezea uwezo taasisi ya Takukuru na kurekebisha sheria ili Takukuru iwe na mamlaka ya kuwafikisha watuhumiwa mbele ya Mahakama bila kuhitaji kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka.
- CHADEMA itahahakisha ajira au teuzi mbalimbali serikalini zitakuwa zinashindaniwa kwa usawa na hivyo kuziba mianya yote ya upendeleo, ikiwa pamoja na uteuzi wa Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi na majaji wengine lazima kwanza uridhiwe na Bunge.
- Maslahi ya watendaji serikalini yataboreshwa ili kila mfanyakazi awe na sababu ya kulinda ajira yake

**Matokeo tarajiwa**

- Nchi kupata katiba ya wananchi itakayoharakisha maendeleo yao na kuwa na Muundo wa Muungano

unaozingatia haki kwa Tanganyika na Zanzibar

- Wananchi wenye kuwajibika na kuwajibishana katika shughuli za maendeleo
- Mapato kuongezeka kutokana na kupunguza matumizi ya serikali na kuzuia ubadhirifu wa fedha za umma
- Nchi kuwa katika **mchakamchaka** *(mwamko, matumaini na hamasa mpya katika utendaji wa kazi)* kuelekea maendeleo ya kweli ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.





**Hali halisi:**

Ili kujenga uchumi imara na kuleta ustawi endelevu wa jamii, wataalamu ni nguzo thabiti katika kufikia malengo haya. Kwa miaka zaidi ya hamsini elimu yetu imeshindwa kukidhi mahitaji ya nguvu kazi katika kuendeleza Taifa letu. Mazingira duni ya kujifunzia, Uhaba wa walimu na vifaa vya elimu vimekuwa ni changamoto kubwa.



*Shule ya awali*

- Elimu ya awali ambayo kwanza inajenga msingi bora na kumuandaa mtoto kuwa mdadisi, mbunifu na mthubutu haijapewa kipaumbele.



Elimu ya msingi:

- Bado watoto hawana madarasa ya uhakika, hawana madawati kabisa au ya kutosha na shule nyingi zina uhaba mkubwa wa matundu ya vyoo.

Sekondari:

- Hakuna maabara, vifaa na wataalamu wa maabara; hakuna maktaba na vitabu vya kutosha; hakuna walimu wa kutosha wenye kiwango cha elimu cha kutosha. Kiwango cha elimu inayotolewa ni duni na haimuandai vya kutosha mwanafunzi kujiajiri na kuajiriwa.

Vyuo:

- Vyuo vinavyofundisha kuongeza thamani ya malighafi mbalimbali kama mazao ya kilimo bado havijatiliwa mkazo. Idadi kubwa ya wanafunzi kuliko miundo mbinu katika vyuo vikuu, wanafunzi wanaofuzu hawana

ujuzi (skills) na hivyo hawana uwezo wa kujiajiri na pia hawaajiriki kirahisi. Ukosefu wa fedha za kugharamia kulipia wanafunzi wote waliofaulu.

*Maswala mtambuka*:

- Walimu wenye ujuzi hasa masomo ya sayansi ni wachache, waliopo hawathaminiwi, hawapewi mafunzo kazini, maslahi duni na hakuna nyenzo za kujifunzia za kutosha.
- Ukosefu wa chakula na lishe kwa wanafunzi hasa elimu ya awali.
- Kutokuwepo na utamaduni wa kujisomea na kuandika.
- Kuna tofauti kubwa katika ubora wa elimu baina ya matabaka ya kijamii hususani katika ufundishaji, vitabu vya kiada na ziada, walimu waliobobea, miundombinu na vifaa vya kujifunzia



**Fursa:**

Ujenzi mkubwa uliofanyika wa shule za kata na vyuo; pamoja na shule na vyuo vya sekta binafsi vinaweza kuboreshwa na kutoa elimu inayokidhi mahitaji ya uchumi na maendeleo ya Taifa letu.

**CHADEMA/UKAWA itafanya nini:**

- Elimu bora itakayogharamiwa na serikali kuanzia elimu ya wali mpaka chuo kikuu kwa kila Mtanzania na hivyo hakuna mtanzania atakayeachwa nyuma.
- Kuanzisha tume au baraza la taifa la Ushauri juu ya elimu likijumuisha wadau wote
- Kuimarisha elimu ya sekondari, teknolojia, ustadi na ufundi inayojenga uwezo wa kujiajiri na ushindani katika soko la ajira.
- Kuimarisha SIDO na vyuo vya ufundi stadi ili kuandaa vijana kuweza kujiajiri.
- Kubadilisha malengo ya jeshi la kujenga Taifa ili lijikite katika kutoa mafunzo ya ufundi na uzalendo.
- Ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya elimu ikiwa ni pamoja na shule za Kata.
- Kusimamia ubora wa viwango vya elimu kote nchini.
- Kuimarisha taaluma na mitaala katika mashule.
- Kutengeneza utaratibu kati ya vyuo vya elimu na sekta binafsi ili vyuo vitekeleze mitaala inayoendana na mahitaji halisi ya waajiri hususani sekta binafsi.
- Kuboresha afya za wanafunzi kwa kupanua programu ya lishe mashuleni kama njia ya kuongeza mahudhurio kati ya wanafunzi na kupunguza utoro.
- Kuboresha maslahi na vitendea kazi kwa waalimu ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kupata nyumba, usafiri na zana za teknolojia.
- Kufuta michango ya maabara ya shule za kata

- Kuimarisha elimu ya watu wazima kwa kuwatumia wanafunzi waliomaliza vyuo ambao hawajaingia kwenye ajira rasmi kufundisha watu wazima.
- Kuwekeza vya kutosha katika tafiti
- Kujenga utamaduni wa kujisomea, kuandika na kutafakari.
- Kutoa elimu bora ambayo itawawezesha Watanzania kushindana kimataifa kwa kuzingatia na kusisitiza masomo ya Sayansi na Tehama.
- Kuanzisha mchakato wa kuona ni jinsi gani Kiswahili kinaweza kuwa lugha ya kufundishia kuanzia elimu ya awali mpaka chuo kikuu.

**Matokeo tarajiwa**

- Elimu bora itakayomwezesha muhitimu kwa kila hatua ya elimu kujitegemea na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi na jamii aliyomo.
- Elimu bora itakayo jenga soko la ajira la ndani na nje kwa vijana.



# AFYA NA HIFADHI YA JAMII



**Hali halisi:**

_Afya_

- Ujenzi wa uchumi imara unategemea sana wananchi wenye afya njema na pia wenye uhakika na matibabu pindi kunapokuwa na mahitaji.
- Ujenzi wa miundombinu ya afya lazima uendane na huduma husika. Baada ya miaka hamsini ya Uhuru, ujenzi wa miundombinu ya afya, mgawanyo wa wataalamu na upatikanaji wa dawa pamoja na vifaa tiba umejikita katika maeneo machache ya nchi, hasa mijini. Hali hii imepelekea kutokuwepo kwa uwiano katika upatikanaji na utoaji wa huduma hizi hapa Tanzania.

- Wananchi wengi bado wanagharamia huduma za afya kwa kutoa pesa mfukoni pindi wauguapo.
- Kupanda kwa gharama za matibabu.
- Magonjwa ya kuambukiza kama UKIMWI na kipindupindu kuendelea kuwa tatizo kubwa na magonjwa yasiyoambukiza kama saratani na sukari kushika kasi miaka ya karibuni kunazidisha umaskini kwa mtu mmoja na Serikali kwa ujumla.
- Serikali kushindwa kugharamia huduma za afya kwa kiwango tarajiwa kutokana na kutenga bajeti isiyokidhi; na ubadhilifu wa fedha chache zinazotengwa kwenye ngazi mbalimbali za utoaji huduma.
- Serikali Kushindwa kuendeleza programu mbalimbali za afya (*mfano mradi wa damu salama)* baada ya wafadhili kumaliza muda wao kunadhorotesha zaidi huduma za afya, kunakopelekea kutokea kwa vifo visivyokua vya lazima.
- Serikali kupoteza fedha nyingi kwa kugharamia matibabu nje ya nchi hasa kwa viongozi na watendaji wa serikali.

*Hifadhi ya Jamii*

- Kwa sasa wazee na wote wasiojiweza wamepangiwa kupata huduma za afya bure ili hali upatikanaji wa tiba na vifaa tiba katika taasisi za umma ni hafifu.
- Wazee na wasiojiweza wamekuwa wakikusanywa kwenye nyumba za matunzo (makambi) na kupatiwa huduma zisizokidhi. Makambi haya yamewafanya wazee kuishi kifungoni na kuwasababishia upweke, msongo wa mawazo, kusononeka na hata sonona.



**Fursa:**

- Kuwepo kwa mifuko ya bima na hifadhi ya jamii.
- Kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi kwenye sekta ya afya katika vyuo vikuu na vyuo vya kati kunatoa fursa ya kupatikana watumishi wengi wa afya.
- Ongezeko la vituo vya afya vinavyoanzishwa na sekta binafsi, pamoja na taasisi za kidini na zile za kijamii.
- Wazee ni kitovu cha busara cha Taifa wanahitaji matunzo bora zaidi.

**CHADEMA itafanya nini:**

- Tutahamasisha idadi zaidi ya Watanzania wajiunge na bima za afya za malipo nafuu.
- Kuimarisha afya ya msingi pamoja na kinga na kuendeleza programu mbalimbali za afya baada ya wafadhili kuondoka.
- Itahakikisha kuna uwiano na upatikanaji wa watumishi wa

afya katika kada mbalimbali ili kuleta tija na huduma stahiki ikiwa ni pamoja na kusomesa kwa gharama ya serikali wataalam bobezi (Specialists) katika fani mbalimbali za afya. Pia wataalamu walio mafunzoni kwa vitendo(kama vile intern doctors, pharmacists, lab scientist, nurses nk) wanaohudumia wagonjwa katika vituo vilivyoainishwa watapatiwa posho za kujikimu ili kuwavutia wataalamu hawa kubaki katika sekta ya afya na kuhakikisha wananchi wengi wanapata huduma kwa haraka.

- Kwa kushirikiana na sekta binafsi, kuimarisha miundombinu ya afya ikiwa ni pamoja na kujenga hospitali za kisasa na kuboresha mifumo ya rufaa ili kusogeza huduma za afya karibu na jamii, kuanzisha utalii wa huduma za afya *(medical tourism)* na pia kuepukana na tiba za nje ya nchi.
- Kurejea kwa lengo la kuboresha maslahi na vitendea kazi katika sekta ya Afya ikiwa ni pamoja na mishahara, nyumba za kuishi na usafiri.
- Kuthibiti ongezeko la gharama za huduma za afya bila kuathiri uendeshaji wa watoaji huduma za afya kama vile serikali na hospitali za sekta binafsi/kijamii/kidini.
- Kuboresha huduma za afya kwa kurejea na kutunga sheria za kusimamia taaluma za afya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na mafunzo endelevu katika taaluma hizo.
- Kuharakisha upatikanaji wa dawa za bei nafuu za magonjwa sugu kama kisukari na serikali kugharamia magonjwa hatarishi "terminal illnesses' kama saratani na UKIMWI.
- Kurejea na kuboresha Taasisi za afya kama MSD, NIMR, TFDA, NHIF ili ziweze kutoa huduma bora na haraka kwa wananchi.

- Kuhamasisha na kugharamia tafiti za afya hasa zinazolenga kuimarisha kinga na kupunguza gharama za huduma za afya.

- Wazee na wasiojiweza watapewa posho ya kujikimu inayokidhi mahitaji ya msingi itakayowawezesha kuishi kwa heshima na kulinda utu wao ndani ya familia na jamii zao. Pia kwa wale wenye matatizo ya macho watapatiwa miwani bure.

- Kuanzisha nyumba mpya na kuboresha nyumba za matunzo ambazo zinahudumia wasiojiweza ambao hawana fursa kuishi na jamii zao.

**Matokeo tarajiwa**

- Wanachi kupata huduma za afya kupitia bima ya afya na mifuko ya jamii bila malipo kutoka mfukoni mwao pindi wauguapo.
- Huduma za afya zitatolewa kwa gharama iliyo rafiki kwa mtumiaji na kwa ubora zaidi.
- Kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaojali afya zao ili kuzuia magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambuzwa.
- Kupungua kwa tatizo la rasilimali watu katika sekta ya afya kupitia ongezeko la vituo vya mafunzo na mafunzo kwa vitendo.
- Watumishi wa afya kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kuwawezesha kutoa huduma bora zaidi.
- Wazee na wasiojiweza kuishi na jamii zao wakiwa na uwezo wa kujikimu ki maisha.



# ARDHI, MAJI ,KILIMO, MIFUGO NA UVUVI



**Hali halisi:**

*Ardhi na Makazi:*

- Ukiritimba wa umilikishaji ardhi kwa ajili ya makazi umepelekea migogoro na taabu ya upatikanaji wa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa makazi, na hivyo kusababisha ujenzi holela mijini na vijijini.
- Wakazi wengi hasa mijini wamepoteza mali na gharama kubwa kutokana na makazi yao kubomolewa bila kulipwa fidia na hivyo kutupwa kwenye lindi la umaskini.
- Wanachi wengi kukaa katika makazi yasiyo rasmi ambayo hayajapimwa na kuwekewa miundo mbinu ya kijamii yanahatarisha maisha ya wakazi wa eneo husika kama kutokea kwa mioto ambayo inaweza isithibitiwe, uchelewashaji wa kufikisha wagonjwa mahututi vituo vya afya n.k.

- Maeneo ya hifadhi kama vile maeneo ya mabonde na ardhi oevu kupimwa kinyemela na mamlaka husika kumepelekea hali hatarishi kwa wakazi wa maeneo husika kama vile kutokea kwa mafuriko katika njia za mifereji au mito yanayosababisha maafa yanayoweza kuzuilika.
- Kutoboresha na kujenga Miundo mbinu ya maji taka mipya na kutegemea iliyochoka *(iliyojengwa wakati wa mkoloni)* hasa sehemu za mijini kumepelekea sio tu kutapakaa kwa maji taka yenye vinyesi pia mafuriko ya mara kwa mara hasa sehemu za mijini.
- Gharama za Vifaa vya ujenzi kuendelea kuwa bei juu siku hadi siku na hivyo kupelekea ukosefu wa makazi bora hasa kwa watu wa vijijini.

*Maji:*

- Tanzania ni nchi pekee barani Africa yenye maji baridi mengi na ya kutosha ikiwa imezungukwa hifadhi kubwa ya maji kila upande; hata hivyo wananchi wake hawapati maji safi na salama. Ni asilimia kumi na tano tu (15%) ya



Watanzania wanaopata maji safi na salama na wengi wao wakiwa mijini.

- ukosekana kwa maji safi na salama kunaleta athari nyingi sana ikiwemo watoto kukosa masomo wakitumia muda mwingi kutafuta maji, uwepo wa magonjwa ya kuambukiza hasa yale ya matumbo, ngozi na upofu.
- Kilimo hubaki kuwa cha kutegemea mvua, na shughuli nyingi hukwama kwa kukosa maji.
- Maji mengi ya mvua yamekuwa yakipotelea baharini bila mkakati madhubuti wa kuyavuna kwa shughuli mbalimbali kama kunywa mifugo, na umwagiliaji.



*Kilimo na Mifugo:*

- Matumizi sahihi ya ardhi huondoa chuki baina ya wakulima na wafugaji na wakazi na wawekezaji kwa upande mwingine. Migogoro ya ardhi hupelekea athari kubwa katika jamii kama vile kuchomeana mashamba na/au makazi na pia hata mauaji ya kutisha.
- Hakuna sera na mikakati ambayoina nia ya hadhi ya kufanikisha kilimo cha kisasa chenye tija kwa watanzania.

- Kuvunjika kwa ushirika kumepelekea kukosekana kwa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo na mifugo.
- Kukosekana kwa mafunzo endelevu katika kilimo na ufugaji kumechangia kwa kiasi kikubwa kudolola kwa sekta hizi.



*Uvuvi:*

Kutokuwepo kwa mafunzo na usimamizi endelevu katika uvuvi na kukosekana kwa mitaji na mafunzo kumepelekea sekta hii kutoa mchango usiokidhi mahitaji katika pato la Taifa. Wananchi kutopatiwa elimu ya kutosha kuhusu uvuvi endelevu kumepelekea mali na zana zao kuharibiwa kama adhabu ya kukiuka sheria, mfano ni uchomaji wa nyavu za wavuvi kanda ya ziwa ambao umechangia umaskini mkubwa katika jamii husika. Kulegalega kwa uvuvi mkubwa hasa wa bahari kuu na kukosekana kwa viwanda vya kutengeneza minofu ya samaki kumepelekea sekta hii kuendelea kudumaa.

**Fursa:**

- Kuwepo kwa ardhi ya kutosha yenye utajiri mwingi wa maliasili.
- Uwepo wa hifadhi kubwa ya maji baridi ya kutosha katika pande zote za nchi.
- Hazina kubwa ya mifugo na ardhi murua inayofaa kwa kilimo.
- Uwepo wa vyuo vya uvuvi vyenye miundombinu ambavyo vikitumiwa vizuri vitasaidia kukuza uchumi wa uvuvi.
- Uwepo wa bahari, mito na maziwa kwa ajili ya uvuvi endelevu.

**CHADEMA itafanya nini:**

*Ardhi na Makazi:*

- Kuimarisha mfumo wa umiliki wa ardhi kwa Watanzania na kudhibiti migogoro ya ardhi hasa kati ya wakulima na wafugaji.
- Serikali ya CHADEMA itahakikisha kila kiwanja kinachopimwa kinakuwa na huduma za maji, umeme na barabara kabla ya mwananchi kumilikishwa.
- Kama ambavyo ilani ya uchaguzi ya CHADEMA ya mwaka 2010 vivyo hivyo ilani hii inaendelea kusisitiza kuwa tutapunguza gharama za vifaa vya ujenzi ziwe na uwiano sawa kwa nchi nzima ili kila mwananchi ajenge nyumba bora na salama na kuondokana na nyumba za tembe na manyasi.
- CHADEMA itapanua miundo mbinu ya maji taka na kujenga mingine mipya ili kuendana na kasi ya ukuaji wa

miji na kupunguza maafa yanatokana na mfuriko pamoja na magonjwa ambukizi

- Tutahakikisha mapato yatokananyo na ardhi na makazi hasa ya kibiashara yanachangia kiasi kikubwa katika pato la Taifa.

*Kilimo:*

- Kutekeleza kilimo cha kisasa na kukinyanyua kikue kwa asilimia sita mpaka nane;
- Kuweka sera na mikakati ambayo itainua hadhi ya kilimo kimapato na kiutendaji ili kilimo kivutie vijana na Watanzania kwa ujumla  na ibadilishe fikra potofu juu ya kilimo;
- Kuhakikisha kwamba wakulima wanaweza kupata mikopo ya muda mrefu ya kuanzia miaka 5 hadi 15 na kuendelea na kwa riba nafuu. Mkakati huu utaimarishwa na msaada kwa wakulima kuunda SACCOS na VICOBA kwa ajili ya kukopeshana wenyewe;
- Kutoa elimu na kuwajengea wakulima miundombinu ya kuendeleza kilimo chao pamoja na miradi ya umwagiliaji na majasho ya mifugo;
- Kuleta mapinduzi ya kilimo kwa kuimarisha elimu, ufundi na teknolojia ya kisasa na kumkomboa mkulima kutoka jembe la mkono;
- Kuwapa wakulima (extension services) maafisa ugani na ushauri wa kilimo cha biashara ili wazalishe kulingana na upatikanaji wa masoko;
- Kuhakikisha upatikanaji kwa wakati wa mbegu bora na pembejeo;

- Kuimarisha na kuongeza vituo vya utafiti katika sekta ya kilimo na kuvipa fungu la fedha litakalo ziwezesha kutimiza mahitaji ya shughuli zao. Tutahakikisha kwamba matokeo na mbegu zinazotokana na vituo vyetu vya utafiti vinakuwa 'commercialized;
- Kujenga maghala zaidi kuhifadhi mazao ya wakulima na tutanua mazao hayo kwa bei ya soko kwa utaratibu wa kulinda bei za mazao hayo kwa wakulima;
- Kuondoa upigaji marufuku wa kuuza mazao ya wakulima nje ya nchi ili kuwapa uhuru wa mahali pa kuuza mazao yao na motisha ya kuzalisha zaidi. Pale inapokuwa lazima Serikali itanunua mazao hayo kwa fedha taslimu kwa bei ya soko na ikitokea kukopa wakati wa kulipa italipa pamoja na riba;
- Ushirika ni nguzo muhimu katika maendeleo ya wakulima na kilimo kwa kuzingatia hilo tutajikita kwenye kujenga na kuimarisha vyama vya ushirika na kuvijengea uwezo ya kutafuta masoko ya mazao yao;
- Kuunda mamlaka itakayokuwa na jukumu la kusimamia mipango na maendeleo ya sekta ndogo ya mboga mboga na maua (horticulture and floriculture) kwa utaratibu wa kuwasaidia na kuwaendeleza wakulima wa sekta hiyo ili sekta hii ifikie mauzo ya mpaka shilingi trilioni nne (USD$ 2 billion) katika miaka yetu mitano ya kwanza ikilinganishwa na kiwango tulichowahi kufikia cha chini ya shilingi trilioni moja (USD$ 500 million);
- Kusimamia kilimo cha biashara kinachozingatia maslahi ya nchi na ya Watanzania.
- Kuanzisha programu maalum ya kufufua mazao asilia ya Tanzania hususani mkonge.

- Tutaweka mikakati ya 'kubrand' mazao ya kilimo ya Tanzania;
- Kusimamia kilimo, ufugaji na uvuvi wa kisasa na kuunganisha sekta hizo na ya viwanda;

*Maji:*

- Kuhakikisha kuwa wananchi wanatunza na kulinda vyanzo vya maji;
- Kuweka mazingira rafiki yatakayowahakikishia Watanzania walio wengi wanapata maji safi na salama;

*Mifugo na Uvuvi:*

- Kufuta kodi zote za mazao na mifugo zisizo na tija kwa wakulima na wafugaji;
- Kuuza nje ya nchi samaki bora.
- Kuanzisha Benki ya Maendelo ya Ufugaji na Uvuvi.

**Matokeo tarajiwa:**

- Mwananchi kunufaika na ardhi katika nchi yake na kuishi katika makazi yaliyo bora yenye hadhi na heshima, na miji iliyopangiliwa vizuri.
- Wananchi kuwa wamiliki wa adhi yao na kufaidika na uwekezaji wowote juu na chini ya adhi (Rasilimali zilizopo ardhini). Matumizi ya adhi yatakuwa kwa ubia na si kwa fidia.
- Kutokuwa na migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, na pia wawekezaji na wananchi.
- Idadi ya wananchi wanaopata maji safi na salama na wanaotumia mfumo maji taka kuongezeka.

# MIUNDOMBINU: RELI, BANDARI, BARABARA, USAFIRI WA ANGA NA USAFIRI WA MAJINI



**Hali halisi:**

*Bandari na barabara:*

- Ujenzi wa miundombinu ya bandari na barabara umekuwa ukiendelea katika sehemu mbalimbali nchini. Bandari za Tanga, Dar es Salaam, Zanzibar na Mtwara zimekuwa zikifanyiwa matengenezo mara kwa mara ili kuleta tija. Ki nadharia bandari hizi zingekuwa nguzo mojawapo kubwa ya uchumi wa Tanzania.

- Sekta ya bandari imeghubikwa na rushwa pamoja na utendaji mbovu kiasi kwamba mrundikano wa mizigo umekuwa mkubwa sana bandarini na kupelekea mapato yake kuwa madogo kulinganisha na fursa za usafirishaji mizigo zilizopo.

- Barabara zimejengwa kwa kiwango cha chini kiasi kwamba hubomoka katika muda mfupi na kuwa ni chanzo cha ajali za barabarani.





*Miundombinu ya Reli:*

Serikali ya CCM imeamua kutelekeza mtandao wa reli na kujikita zaidi kwenye usafirishaji wa mizigo nchi kavu kwa kutumia njia ya barabara. Hali hii imeongeza gharama za usafirishaji, uharibifu wa barabara na kusababisha kutokea kwa ajali mbaya mara kwa mara na kudumaza uchumi wa nchi.



*Usafiri wa Anga:*

Shirika la ndege la Tanzania lilikuwa ni shirika lenye ufanisi mkubwa katika usafiri wa anga barani Afrika. Hata hivyo shirika hili kwa sasa lina chechemea likiwa na watumishi wengi na likitegemea Hazina kulipa mishahara.




*Usafiri wa Majini:*

Usafiri wa majini umekuwa ni tatizo sugu ambalo linahitaji mkakati wa haraka katika maeneo yote yanayohitaji usafiri huo hasa maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika maziwa haya Vivuko ni vya kizamani na havitoshi na meli zilizopo ni mbovu sana. Hii inapelekea wananchi kutegemea mitumbwi na njia zingine mbadala ambazo ni hatari kwa maisha yao na pia wanashindwa kufanya shughuli za kiuchumi kama usafirishaji wa bidhaa.

**Fursa:**

- Ujirani na nchi nyingi zisizo na bandari, kunatoa fursa kwa Tanzania kujenga uchumi wa bandari na usafirishaji.

- Uwepo wa malighafi nyingi za mazao ya kilimo na mifugo zinatoa fursa ya kukuza miundombinu ya usafirishaji.
- Tanzania kuwa nchi mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kimataifa, hivyo kuongezeka kwa huduma ya usafirishaji.
- Kuwa na fukwe za bahari na maziwa yenye mandhari inayohitajika kujenga bandari.
- Kuwa na akiba (deposit) ya kiasi kikubwa cha chuma na fursa ya kuzalisha kiasi kikubwa cha nishati nyingi na ya bei nafuu
- Kuwepo na wasafiri wengi wa ndani na nje kunatoa fursa ya kuwekeza katika usafiri wa anga.

**CHADEMA itafanya nini:**

- Kujenga reli mpya na kukarabati zilizopo kwa viwango vya kisasa kwa kuzingatia maslahi ya nchi . Hii ni pamoja na kujenga uwezo wa kuzalisha mataluma ya reli nchini.
- Kuboresha bandari zilizopo na kujenga mpya kama vitega uchumi vya Taifa ili kurejesha biashara tulizopoteza kwa bandari za nchi jirani.
- Kujenga barabara nchini kwa kuzingatia ubora hasa zile za vijijini.
- Kujenga shirika la Ndege la Taifa linalojiendesha kwa misingi ya faida.
- Kujenga miundombinu ya kisasa ili kuondoa misongamano ya magari hasa katika majiji ya Dar es salaam, Mwanza,

Mbeya, Arusha na miji mingine inayokuwa kwa kasi nchini.

- Kuimarisha usafiri wa majini kwa kuboresha na kuweka miundo mbinu mipya.

**Matokeo tarajiwa:**

- Bandari kuwa njia kuu ya uchumi kwa kuhudumia kilimo na viwanda. Na pia, kuchangia zaidi ya theluthi moja ya pato la Taifa.
- Shirika la ndege la Taifa (Air Tanzania) kuimarishwa ili kutoa huduma nchini na nje ya nchi huku likijiendesha kibiashara zaidi na kwa fiada.
- Wananchi hasa wa visiwani kupata huduma muhimu za kiuchumi na kijamii.
- Mizigo yote mizito kusafirishwa kwa njia ya reli na meli ili kupunguza gharama na kuongeza tija katika uzalishaji. Kupunguza ajali na kulinda miundo mbinu.
- Barabara zinazodumu na zilizo salama zaidi kwa watumiaji.



# VIWANDA



**Hali halisi:**

- Chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, viwanda vingi vilijengwa vilivyowezesha kwanza kuwa soko la mazao na malighafi mbalimbali nchini, kuzalisha bidhaa nzuri hapa nchini na hivyo kupunguza uagizaji bidhaa kutoka nje kulikoimarisha thamani ya shilingi yetu. Sekta ya viwanda tulipopata uhuru ilikua ikichangia takribani asilimia tisa ya pato la taifa.
- Viwanda hivi kama vile vya nguo, ngozi, zana za kilimo, silaha, kufua chuma vilitoa ajira kwa watu wengi hasa vijana.
- Ubinafsishaji ambao haukuwa na tija kwa Taifa umepelekea viwanda vingi kati ya hivyo kutozalisha

na badala yake vimegeuka maghala (godowns) ya bidhaa kutoka nje ya nchi na vingine vimefungwa kabisa. Hii imechangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa ajira, watanzania kuwa wachuuzi na hata kushuka kwa shilingi ya Tanzania.



**Fursa:**

Malighafi mbalimbali za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu, madini n.k na soko kubwa la bidhaa lililopo nchini linatoa fursa ya serikali kuwekeza katika viwanda vidogo na kati.

**CHADEMA itafanya nini:**

Tutainua mchango huu wa sekta hii muhimu ufikie siyo chini ya asilimia kumi na tano (15%) katika miaka yetu mitano ya kwanza. Tutafanya hivyo kwa:

- Kuimarisha sekta ya viwanda kuwa mhimili wa uchumi kwa uzalishaji wa bidhaa na ajira endelevu;
- Kujenga viwanda vipya vya kusindika mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji;
- kuingia mikataba ya kuleta technologia ya kutengeneza bidhaa badala ya kuleta bidhaa;
- Kuhakikisha kuwa ndani ya miaka mitano asilimia **(75%)** ya mali ghafi zote za Tanzania zinasindikwa kabla ya kusafirishwa nje ili kuongeza mapato na ajira ya mamilioni ya vijana;
- Kutoa kipaumbele na vishawishi maalum kwa viwanda vya kuendeleza kilimo. Kwa mfano, tutaendeleza viwanda vya mbolea kulingana na mahitaji ya taifa na uuzaji wa ziada ya bidhaa hiyo nje ya nchi; pili viwanda vya kutengeneza mbegu bora na madawa ya kilimo;
- Kupiga marufuku uuzaji wa korosho ambazo hazijabanguliwa na kuhakikisha kwamba asilimia mia moja ya korosho zote tunazozalisha (zaidi ya tani laki mbili) zitabanguliwa hapa Tanzania na kuuzwa kwa walaji wa ndani na nje;
- Kupiga marufuku uuzaji nje ya nchi ngozi ambazo hazijasindikwa na kuhakikisha kwamba zinaongezewa thamani ya kuziwezesha zizalishe bidhaa zote zinazotokana na ngozi;
- Kufufua na kuongeza viwanda vyetu vya nguo ili tuweze kusindika kiwango kitachofikia asilimia sabini na tano (75%) ya pamba inayozalishwa Tanzania.
- Kuimarisha na kukuza usindikaji wa mazao ya katani,

kahawa, tumbaku na chai ili kuhakikisha ongezeko kubwa la thamani katika mazao haya na ongezeko kubwa la bidhaa zinazotokana na mazao haya.

- Kuanzisha Benki ya Ukuzaji wa Viwanda.

**Matokeo tarajiwa**

- Kuwepo kwa Soko kubwa la malighafi mbalimbali za kilimo, uvuvi, ufugaji, misitu n,k
- Vijana wengi kupata ajira katika viwanda vidogo na vikubwa vitakavyojengwa
- Kuongezeka kwa mauzo ya nje na kupungua uingizwaji wa bidhaa kutoka nje
- Kukua kwa uchumi endelevu.

# UCHUMI SHIRIKISHI, BIASHARA, FEDHA NA MITAJI



**Hali halisi:**

Tanzania ina raslimali ya kutosha kuondoa umaskini lakini ili mchakato huu ufanikiwe unahitaji kutumia kwa kiwango cha juu raslimali watu na mali asili kwa manufaa ya Watanzania wote.

Tunatambua kwamba maendeleo ya Tanzania na Watanzania lazima yaletwe na Watanzania wenyewe kwa kuelewa kwamba wawekezaji kutoka nje watachangia na kuongezea juhudi za Watanzania hususani kwa ubia kati yao na Watanzania.

Tanzania ni nchi yenye uchumi mdogo ila ikipania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Endapo itaendelea na mfumo wa utawala tulionao usio na mipango, mikakati na usimamizi makini wa ukuaji wa uchumi, basi dhamira hii ya

kuwa nchi ya uchumi wa kati haitatimia.

Matatizo yetu ya uchumi yapo katika maeneo makuu yafuatayo:

- Uwezo mdogo wa kitaifa wa uzalishaji mali wenye tija.
- Matumizi mabaya ya fedha za umma.
- Serikali kuwa na wigo mfinyu wa kukusanya kodi. Na pia, kutokukusanya kodi ipasavyo hivyo kushindwa kuongeza mapato.
- Madeni na mikopo isiyo na tija kwa maendeleo endelevu.
- Kukosekana kwa viwanda vya uzalishaji na uchakataji malighafi kulikosababishwa na kuua viwanda vilivyokuwepo, kudhoofisha viwanda vya ndani, na kutojenga viwanda vipya kulingana na mahitaji ya Taifa.
- Uchumi kuwa dhaifu kutokana na kushindwa kutumia vizuri raslimali asilia.
- Sekta binafsi ya watanzania haijawekewa mazingira mazuri ya kukua na kuchangia pato la taifa.



**Fursa:**

- Kuwepo kwa rasilimali watu na malighafi za kutosha nchini.
- Idadi kubwa ya watu inayotoa wigo mpana wa biashara.
- Soko la mitaji na mabenki.
- Utulivu wa kijamii.
- Ujirani mwema wa Tanzania na nchi inayozizunguka.

**CHADEMA itafanya nini:**

Kubadili kwa mfumo wa Uchumi wa nchi ili kuhakikisha kuwa mfumo wa uchumi wa Tanzania unakuwa ni wa soko-jamii (social market economy), ambapo nguvu za soko zitatumikia jamii kwa serikali kuweka uwiano wa mapato unaohakikisha huduma za kijamii zinapatikana kwa ufanisi.

- Kubuni na kutekeleza mpango kabambe ili kuwawezesha Watanzania kushiriki katika nyanja zote za uchumi kwa lengo la Watanzania kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wa taifa ikiwa ni pamoja na kuwepo upendeleo maalum ili wafikie lengo hilo.
- Katika uwekazaji: Kudumisha na kutekeleza mazingira mazuri ya uwekezaji kwa sekta binafsi yenyewe na kwa maeneo ambayo sekta binafsi inashirikiana na sekta ya umma au Serikali. Utekelezaji huu utakuwa ni pamoja na kodi nafuu zinazo shindana na washindani wetu wa kiuchumi; kuondoa urasimu unaoambatana na rushwa katika vibali vya uwekezaji; na kuondoa matatizo na vikwazo vinavyotokana na taasisi za udhibiti.
- Kuwawezesha Watanzania kupata mitaji ya biashara kwa masharti nafuu kabisa.

- Kuvutia uwekezaji na wawekezaji wenye tija. Kuweka udhibiti wa wahamiaji wasioleta tija wala maslahi kwa Taifa.
- Kuimarisha sera ya ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi kwenye maeneo muhimu ya kiuchumi na kibiashara. Pia, kuwawezesha Watanzania kuwekeza kwa njia ya ubia na wawekezaji wenye mitaji mikubwa kutoka mataifa mbalimbali duniani.
- Kuimarisha usimamizi kwa kubadilisha mfumo wa Vyama vya Ushirika nchini ili utokane na uendeshwe na wakulima wenyewe ikiwa na pamoja na kuwawezesha kuboresha makazi kwa mpango wa kushirikiana kujenga nyumba bora
- Kuwezesha uanzishaji wa viwanda[1] vidogo vidogo na vya kati vinavyotoa ajira kwa wingi kwa kuvihusisha na vyuo vya ufundi na benki maalum kwa lengo hilo.

**Matokeo tarajiwa:**

- Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025. Hii ina maana kwamba, unakuwepo uwiano wa haki kimapato unaomwezesha kila mwananchi kupata huduma za kijamii kwa ufanisi.
- Kila Mtanzania kutumia rasilimali zake kwa ubia badala ya kuuza. Kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika soko la mitaji.
- Serikali isiyo na madeni yanayodidimiza maendeleo ya uchumi wa Taifa (Deni la ndani lisizidi **asilimia 1** ya pato la Taifa).
- Wazabuni wote wa ndani kulipwa kwa wakati.

1 Kuhamasisha wawekezaji wa ndani kuingia ubia na nje ili kukuza mitaji na teknolojia.

- Ushirika ulioimarika na wakulima kupata mapato ya uhakika kila mwaka kutokana na uuzaji wa mazao yao bila kukopwa.
- Kuwepo kwa makampuni ya Kitanzania yenye mitaji mikubwa yanayojiendesha kibiashara ndani na nje ya nchi (Ongezeko la usafirishaji bidhaa nje ya nchi).
- Kukua na kuimarika kwa kinga za biashara, kwa kupanua wigo wa bima. Serikali na sekta binafsi zikishirikiana kuweza katika usalama na uhakika wa biashara mbalimbali.





# NISHATI, MADINI, GESI NA MAFUTA



**Hali halisi**

<u>*Nishati kwa matumizi ya kawaida na uzalishaji*</u>

- Mrundikano wa kodi katika nishati (gesi, mafuta na umeme) unaopelekea nishati hizi kuwa ghali kwa matumizi ya kawaida na ya uzalishaji na hivyo kuongeza gharama za maisha na kuchochea umaskini.
- Serikali ya CCM inaporuhusu ushiriki wa sekta binafsi usio na kikomo inasababisha sekta ya uzalishaji mkubwa wa umeme uwe mikononi mwa wageni ambao wanadhibiti vianzio na kuinyima serikali uwezo wa kuwa na uhakika wa uwepo wa umeme ambao ndio kivutio kwa wawekezaji kwenye uzalishaji mali, hasa viwanda.
- Vipaumbele havijawekwa kwenye uendelezaji wa vianzio vya uzalishaji umeme wa bei nafuu vilivyopo nchini ; mfano Stiglers (kwenye bondo la mto Rufiji)

- Umeme hausambazwi kwa vipaumbele mfano maeneo ya uzalishaji kama viwanda.
- Hakuna mpango madhubuti wa kusambaza gesi asilia iliyogundulika kwa wingi hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya majumbani na viwandani kote nchini.



*Madini*

- Raslimali ya madini huisha kabisa iwapo itavunwa bila mipango madhubuti na hivyo uvunaji wake unahitaji uwe endelevu kwani ni urithi wa vizazi vyote vya watanzania.
- Serikali ya CCM haijabuni matumizi sahihi na endelevu ya mapato yatokanayo na utafutaji na uchimbaji wa madini (exploration and production) kwa faida ya watanzania.
- Serikali ya CCM imesababisha uwepo wa mikataba mibovu ya madini; na mikataba ya uzalishaji mkubwa

wa umeme inayopendelea wawekezaji wa kigeni dhidi ya maslahi ya Taifa kutokana na kutokuwepo kwa ushirikishwaji wa watanzania kupitia Bunge lao tukufu kwenye maamuzi husika. Na mikataba hiyo hufanywa kuwa siri ya Serikali na wawekezaji.



*Gesi na Mafuta*

- Katika miaka ya hivi karibuni nchi yetu imeingia katika historia mpya ya uvumbuzi na ugunduzi wa kiwango kikubwa cha gesi na taarifa za Serikali zinaonyesha kuwa hadi sasa kuna futi za ujazo trilioni 52. Watafiti wanakwenda mbali zaidi wakisema kuna kiwango kikubwa zaidi (mara nne) cha nishati hiyo nchini kote, hasa katika maeneo ya ukanda wa pwani ya bahari na nchi kavu.
- Shughuli za utafutaji mafuta katika kina kirefu baharini ulianza mwaka 1999 na takwimu zinaonyesha dalili nzuri za kuwepo kwa maeneo (structures) yanayoweza kuhifadhi mafuta na gesi.

*Changamoto mtambuka*

- Utafutaji na uchimbaji madini na utafutaji wa gesi na mafuta kuwa mikononi mwa sekta binafsi ya kigeni bila

kuzingatia uimarishwaji wa sekta binafsi ya kiTanzania isiyoweza kushindania fursa hiyo.

- Serikali ya CCM inawalipisha wazawa na wageni ada na kodi sawa kwenye sekta ya madini, gesi na mafuta.

**Fursa**

Uwepo wa kiasi kikubwa cha madini na vyanzo vya nishati hapa nchini.

**CHADEMA itafanya nini**

- Tutalenga kuongeza 3,000 MW katika gridi ya taifa katika miaka yetu mitano ya kwanza kwa kutumia umeme wa maji na gesi ambazo vyote vitakuwa na gharama nafuu kwa maendeleo ya viwanda na matumizi ya nyumbani ukiweka maanani kwamba wakati nchi kama Misri inalipiza gharama ya centi 2 za dola za kimarekani kwa KWH Tanzania ni centi 16 za dola za kimarekani kwa KWH na wakati huo huo hatuna budi kushindana nan chi kama soko la pamoja.
- Tutaimarisha uzalishaji na usambazaji wa umeme ili kufikia zaidi ya asili mia **(75%)** ya Watanzania wote mijini na vijijini.
- Tutalenga kupunguza matumizi ya nishati ya misitu kama kuni na mkaa kwa asilimia themanini kwa kuongeza matumizi ya nishati mbadala kama gesi asilia, mkaa wa mawe na nishati jadidifu.
- Uzalishaji wa nishati ya kutosha na bei nafuu; na matumizi yenye tija ya madini na nishati
- Kupunguza bei ya mafuta, gesi na umeme kwa matumizi ya kawaida na uzalishaji kwa kupunguza mrundikano wa kodi  na urasimu wa upatikanaji wake ili kupunguza gharama za maisha kwa Watanzania.

- Serikali ya CHADEMA (yenyewe au kwa ubia na makampuni ya uzalishaji wa nishaji) kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa nishati.

- Itatengeneza mazingara mazuri ya kisera yatakayovutia na kuwezesha ushiriki wa Watanzania  na ubia na wageni.

- Serikali ya CHADEMA itaupa uzalishaji mkubwa wa umeme wa maji kipaumbele namba moja, umeme wa makaa ya mawe kipaumbele namba mbili, umeme wa gesi asilia kipaumbele namba tatu na umeme wa urana kipaumbele namba nne. Pia itaupa uzalishaji mdogo na kati wa umeme maji na takataka kipaumbele namba moja, makaa ya mawe na mionzi ya jua kipaumbele namba mbili na wa joto la dunia kipaumbele namba tatu.

- Serikali ya CHADEMA itatoa vipaumbele muhimu kwenye usambazaji wa huduma kubwa ya umeme sehemu za uzalishaji uliyolenga masoko ya ndani na nchi jirani.

- Serikali ya CHADEMA itatunga sheria madhubuti dhidi ya uthubutu na kujihusisha na vitendo vya rushwa na ukwepaji kulipa kodi, na wale wote wataohusika na rushwa na ukwepaji kodi kwenye biashara ya nishati na madini hapa nchini. Pia tutapitia mikataba yote ya nishati ya mafuta na gesiasilia, umeme na madini na kwa kushirikiana na wawekezaji wahusika tutayaboresha kwa manufaa ya Watanzania wote.

- Tutaendeleza utafiti madhubuti wa mafuta na gesi ili kuhakiki akiba tulionayo.

- Tutahakikisha kwamba Watanzania wanashirikishwa katika ngazi zote za utafutaji, uchimbaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia
- Serikali ya CHADEMA itatumia sehemu ya hisa zake kwenye raslimali kubwa ya gesi asilia iliyopo hapa nchini kama dhamana ya kuboresha miundo mbinu na kuwekeza katika miradi mikubwa ya maendeleo ya Taifa
- Tutaweka utaratibu maalum wa kusaidia na kuendeleza wachimbaji wadogo wadogo katika ngazi mbalimbali za uendelezaji wa juhudi zao ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za leseni zao na kuwasaidia kuweza kutathimini madini waliochimba ili wapate bei nzuri/stahili.
- Tutajenga mazingira ya kuwawezesha Watanzania kushiriki katika miradi mikubwa ya madini mbalimbali ikiwepo pamoja na utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani. Tutatoa vishawishi maalum vya kuwezesha uwekezaji.
- Serikali ya CHADEMA itatoza Watanzania wanaoshirikiana kibiashara na wageni (kwa ubia) ada na kodi ndogo zaidi ya zinazotozwa kwa wageni wasiowekeza kwa kushirikisha wazawa.
- Itasitisha utoaji wa misamaha ya kodi kwenye sekta ya madini, na badala yake itawekeza kwenye kuongeza thamani ya rasilimali zake za madini na ujenzi wa miundombinu wezeshi, utafutaji na uchimbaji wa madini kwenye ushindani wake na nchi nyingine kwa kuvutia wawekezaji.

- Serikali ya CHADEMA itawekeza katika kuwawezesha zaidi vijana wetu wasomee taaluma hiyo katika maeneo ya uhasibu, mikataba, majadiliano, sera ili kuepuka hatari ya kuingia makubaliano yasiyokuwa na tija kwa taifa.
- Serikali ya CHADEMA itawekeza mapato yake yote yatokanayo na utafutaji na uchimbaji madini hapa nchini kwenye mfuko maalum wa kitaifa utakaokuwa ukitoa mikopo yenye riba nafuu kwa Serikali na sekta za umma na binafsi kwa ajili ya kuwezesha harakati za kitaifa za kujitafutia maendeleo ya kiuchumi, na kuwekeza kwenye biashara za kimataifa zilizo mihimili mikuu ya maendeleo endelevu yatokanayo na gunduzi za kisayansi na kiteknolojia, na matumizi yake kwenye ujenzi wa chumi za Dunia.
- Kutokana na ukubwa wa majukumu katika wizara ya nishati na madini, serikali ya CHADEMA itaanzisha wizara maalumu ya kushughulikia nishati, Gesi na Mafuta.

**Matokeo tarajiwa**

- uzalishaji wa nishati ya kutosha na bei nafuu; na matumizi endelevu na yenye tija ya madini na nishati kwa kizazi cha sasa na kijacho.



# MALI ASILI NA UTALII



**Hali halisi:**

*Wanyamapori, vivutio vya utalii*

- Pamoja na kuwa utalii ni moja wapo ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa, bado maliasili zake hazijatumiwa vya kutosha ili kuongeza zaidi pato la Taifa, kutokana na mianya mingi kwa makampuni ya kitaalii ya ndani na nje kukwepa kodi ambayo ingepaswa kuingia katika mfumo wa Taifa.
- Hata kipato kidogo kinachopatikana katika utalii kinatishiwa na ujangili wa kuua Tembo na Faru, na uharibifu wa mazingira maeneo ya vivutio vya utalii kunakopelekea uwezekano wa utalii kutokuwa endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho.



*Misitu*

- Misitu ya asili na ambayo huchukua muda mrefu katika ukuaji wake kama mninga inapungua kwa kasi sana na karibu inatoweka kabisa katika ardhi ya Tanzania. Tatizo kubwa ni kuwa misitu hii inavunwa kiholela na uvunaji wake hauna tija kwa Taifa; mfano ni misitu iliyo mipakani mwa nchi jirani ambayo imekuwa ikivunwa na wageni wa nchi za jirani kwa kushirikiana na mamlaka za ndani katika maeneo husika. Na wakati haya yote yakitokea kasi ya upandaji wa miti mipya na hata miti kwa ajili ya uzalishaji wa nishati imekuwa ikisuasua na hivyo kuiweka nchi yetu katika hali hatarishi kugeuka kuwa jangwa.

Hakuna mipango mizuri na uvunaji endelevu wa misitu na utengenezwaji wa samani bora zaidi zitakazoweza kuuzwa nje.

**Fursa:**

- Bado kuna maeneo makubwa yenye maliasili adimu ambayo yanaweza kutunzwa sasa kwa ajili ya vizazi vijavyo
- Maazimio na mikakati mbalimbali ya kuzuia uvunaji haramu wa maliasili za nchi kama pembe za ndovu na magogo yanayochukuliwa na mataifa makubwa kama China yanaweza kuzuia ujangili/uharamia huu kwa huko ndiko soko la maharamia lilipo.

**CHADEMA itafanya nini:**

- Kusimamia uvunaji na matumizi ya rasilimali za Taifa kwa manufaa ya kila Mtanzania wa kizazi hiki na kijacho
- Kupiga vita ujangili na kuimarisha utunzaji wa hifadhi za taifa na mazingira
- Kuchochea ujenzi wa miundombinu ya utalii nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mahoteli na kuimarisha mafunzo
- Kuingia mikataba ya kimataifa kupitia UN ya kupambana na ujangili kwenye hifadhi, mbuga na masoko.
- **Kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni mbili katika miaka mitano**

**Matokeo tarajiwa**

- Mapato yatokanayo na utalii na uuzwaji wenye tija wa magogo kuongezeka
- Kuuza nje samani zenye ubora wa hali ya juu na hivyo kupata mapato endelevu
- Kupunguza uhalibifu wa mazingira
- Kulinda vyanzo vya mito



# AJIRA, VIJANA NA WANAWAKE




**Hali halisi**

- Ajira ni tatizo kubwa kwa sasa hapa nchini. Vijana wengi wanaomaliza vyuo hawapati ajira za uhakika. Uchumi dhaifu na mipango mibovu kwa vijana imepelekea vijana wengi kuwa wachuuzi wa bidha kutoka nje badala ya kujiajiri au kuajiriwa katika sekta rasmi yenye kipato cha uhakika.
- Vijana hawajawekewa mazingira ya kuonyesha na kutumiwa vipaji vyao,
- Elimu ya kujikinga na maradhi hasa yanayoambukiza bado haijawafikia vizuri vijana
- Unyanyasaji wa wanawake katika masuala ya mirathi na talaka bado unaendelea.

- Haki za watoto ikiwepo haki ya kuishi katika mazingira ya amani, kusoma na kutambuliwa utoto wake bado ni tatizo.
- Vyombo vya burudani bado haviheshimu haki za familia kulea watoto wao pasipo kuwaonyesha watoto burudani ambazo zimekusudiwa kwa watu wazima.
- Mimba za utotoni bado ni tatizo
- Matumizi ya nguvu majumbani na ya vuguru za kijinsia *(Gender Based Violence)*. Bado ni tatizo
    - Ubakaji ndani ya ndoa/mahusiano hautambuliwi kuwa ni kosa la jinai.
    - Matumizi ya nguvu na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wasaidizi wa majumbani ambao wengi ni wanawake.



**Fursa**

- Utayari wa serikali ya UKAWA kupitia CHADEMA kama ushirikiano unaojali haki na usawa katika familia na jamii kwa ujumla
- Uwepo wa asasi za kiraia zinazoshughulika na mambo ya kijinsia kutawezesha uharaka wa kutungwa kwa sheria/sera mbalimbali za kulinda wanawake na watoto



**CHADEMA itafanya nini**

- Kutekeleza sera na mkakati ambao utatuwezesha kutoa ajira ambazo zitafikia milioni kumi kwa miaka yetu mitano ya kwanza.
- Kuhakikisha kuwa vijana wanapata elimu ili waweze kutengeneza mazingira ya kujiajiri na kuajiriwa.

- Ili kutumia vipaji mbalimbali kutengeneza ajira CHADEMA itaanzisha mamlaka ya Uratibu wa Ajira ya Tanzania [Tanzania Employment Regulatory Authority-TERA] itakayokuwa na ofisi kila halmashauri kuratibu "innovative industrial incubators" ambapo vijana watapatiwa mafunzo ya uzalishaji, biashara na kupewa mikopo isiyokuwa na masharti magumu yenye bima itakayokatwa na mamlaka na dhamana ya serikali ya mitaa, kuingia ubia kati ya umma na sekta binafsi ili kukuza vipaji na kuongeza ajira kwa kundi kubwa la vijana
- Kusimamia haki za wanawake na kuimarisha ushiriki wao katika uchumi wa upendeo maalum
- Kuimarisha ushiriki wa wanawake katika uongozi wa nchi ili kufikia kiwango cha asili mia hamsini (**50% kwa 50%)** ifikapo 2020
- Ili kuwawezesha wanawake kuunganisha nguvu zao bila kujali tofauti zao za kisiasa, dini, uchumi, kabila n.k., Serikali ya CHADEMA itaruhusu na kufanikisha kuanzishwa kwa Baraza la Wanawake Tanzania. Baraza hili litakuwa chombo huru cha kutetea maslahi ya wanawake na wote nchini.

**Matokeo tarajiwa**

- Wanawake, watoto na vijana kulindwa kisiasa, kijamii na kiuchumi
- Wanawake, watoto na vijana kuishi kwa heshima stahiki katika nchi yao
- Vijana kuwa na ajira za kutosha na kushiriki kikamilifu katika kuendeleza uchumi wa nchi yao



# SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO



**Hali halisi:**

- Pamoja na kuwa Tanzania kwa sasa inazidi kung'aa kupitia wasanii wa muziki wa kizazi kipya katika anga za kimataifa, Juhudi kubwa haijawekwa katika kukuza na kuendeleza sanaa, utamaduni na michezo. Kazi za wasanii bado hazilindwi, mazingira mazuri kwa wasanii kufanya kazi zao hayajawekwa na hivyo kupelekea hali duni ya maisha kwa wasanii hasa uzeeni
- Timu zetu za mipira bado hazifanyi vizuri kimataifa na pia vipaji vingine kama riadha havijawekewa mikakati.
- Utamaduni wa kigeni unazidi kutamaraki nchini siku baada ya siku na kuonyesha hatari ya kupeteza utamaduni wetu kabisa.




<u>*Maswala mtambuka*</u>:

Elimu ya sanaa, utamaduni na michezo haijawekezwa vya kutosha

**Fursa:**

- Uwepo wa vijana wenye vipaji mbalimbali na wenye kujivunia utamaduni wetu
- Kukubalika kwa lugha ya kiswahili ndani na nje ya bara la Afrika
- Jiografia na hali ya hewa ya Taifa letu
- Jamii kubwa ya watanzania kupenda sanaa, michezo na burudani

**CHADEMA itafanya nini:**

- Kubaini, kuendeleza na kuwezesha vipaji vya sanaa na michezo
- Kurudisha, kutenga viwanja vya michezo
- Kufuta kodi zote za vifaa vya michezo.
- Kudhibiti viwango na maadili ya bidhaa za nje zinazoingizwa nchini na kuzitoza kodi halisia
- Kujenga taasisi na vyuo vya kukuza michezo ili kuhakikisha kuwa ndani ya miaka mitano Tanzania inashiriki kwa ushindi katika mashindano ya kimataifa ya soka na riadha
- Kulinda Hakimiliki za sanaa
- Kufuta kodi za sanaa kwa wasanii chipukizi
- Kukuza lugha ya kiswahili kwa kuandaa walimu wengi wa kufundisha kimataifa

**Matokeo tarajiwa**

- Sanaa na michezo kuwa ajira endelevu kwa vijana
- Kulinda na kutunza utamaduni wa mtanzania
- Kuongeza pato la Taifa



# ULINZI, USALAMA NA HAKI ZA RAIA



**Hali halisi:**

<u>*Vyombo vya ulinzi na usalama*</u>:

- Tanzania imekuwa ikifurahia utulivu na amani kwa zaidi ya miaka hamsini sasa. Majeshi yetu ya ulinzi na usalama yamekuwa mstari wa mbele kusaidia jamii na kuhakikisha kuwa kuna hali ya utulivu. Pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuhakikisha kwamba ulinzi na usalama unakuwepo, changamoto kadhaa inabidi zifanyiwe kazi kama vile; Kuendelea kuzorota kwa mahusiano kati ya askari Polisi na raia na kupungua kwa usalama wa polisi katika maeneo yao ya kazi kama ambavyo matukio ya hivi karibuni yalivyojionesha.
- Pamoja na kazi kubwa na yenye hali hatarishi wanayofanya watumishi wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama watumishi hawa ambao ni Wanajeshi, Mapolisi, Askari Magereza, wamekuwa hawathaminiwi na kuendelea

kuishi maisha duni hasa kutokana na:

- *Kupewa mikopo yenye riba ya juu sana tofauti na watumishi wengine ambapo riba hii hupelekea wao kubaki na mishahara midogo mwisho wa mwezi kwa sababu ya kulipa madeni mengi.*
- *Posho ya Chakula (Ration allowance) kuwa kidogo sana kulinganisha umuhimu wa kazi yao na mazingira hatarishi wanayofanyia kazi.*

- Kutokuwepo eneo la tukio kwa wakati kutokana na miundombinu isiyokidhi, na pia kukosekana kwa dhamira ya dhati ya kisiasa katika kuimarisha sekta ya ulinzi na usalama hasa ajali za moto, mafuriko na kadhalika kumepelekea upotevu wa mali na vifo visivyokuwa vya lazima.
- Ukosefu wa vifaa na weredi katika Usalama wa usafiri majini imekuwa changamoto kubwa na hivyo kupelekea ajali mbaya za majini kama zile zilizotokea Zanzibar miaka ya karibuni.





*Mahakama*

- Katika mfumo wa mahakama kuna ucheleweshaji wa utoaji haki kwa raia na hivyo kupelekea magereza na mahabusu kuwa na msongamano usiokuwa wa lazima.
- Miundo mbinu ya majengo hasa mahama za mwanzo ni duni hivyo kuwafanya watumishi wa kimahakama kufanya kazi katika mazingira magumu.

**Fursa:**

- Jeshi latu limekuwa lenye nidhamu kubwa na uzalendo wa hali ya juu.
- Nafasi yetu kijiografia inatuweka katika hali ya utayari katika kujilinda.
- Idadi kubwa ya vijana wakakamavu na wenye usikivu wa hali ya juu.
- Mabadiliko ya Katiba kuelekea katika uundwaji wa katiba ya wananchi, itahakikisha haki na utu wa binadamu unalindwa.

- Dhamira ya serikali ya CHADEMA/UKAWA kuboresha haki za Raia na wafungwa

**CHADEMA itafanya nini:**

- Ili majeshi yetu yote yaweze kufanya kazi kwa ufanisi bila kuwa na maisha magumu yanayotokana na mrundikano wa madeni , serikali ya CHADEMA itaweka utaratibu wa kukopa kwa riba nafuu kwa watumishi wote wa vyombo vya dola sambamba na uboreshwaji wa maslahi yao kwa ujumla.
- Serikali ya CHADEMA itaongeza posho ya chakula (ration allowance) kwa watumishi wa vyombo vyetu na itahakikisha posho hii haikatwi kwa wale wanaoenda mafunzoni.
- Kujenga upya mfumo wa kulinda na utoaji haki katika kila ngazi ikiwemo polisi, mahakama na magereza.
- CHADEMA itatoa na kuimarisha mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wa vyombo Ili kupunguza matumizi yasiyo rasmi na yale yasiyokubalika ya vyombo vya ulinzi na usalama hasa katika shughuli za kisiasa.
- Kupiga vita rushwa na matumizi maba ya ya madaraka katika vyombo vinavyosimamia haki za raia.
- Kuondoa na kupiga vita mifarakano ya kidini, na kuhakikisha kuwa watu wote wanaishi kwa kuheshimiana.
- Kufanya mapitio ya mafunzo, maslahi na vitendea kazi kwa vyombo vya ulinzi na usalama.
- Kuimarisha na kujenga mfumo endelevu wa uhusiano na ushirikiano baina ya raia na vyombo vya ulinzi na usalama nchini.



**Matokeo tarajiwa:**

- Kutengeneza Mahusiano mema kati ya raia na vyombo vya ulinzi na usalama nchini.
- Kuwa na Majeshi la kisasa na yanayoitikia kwa wakati na umakini ili kufikia malengo tarajiwa.
- Kukua kwa biashara na uchumi kutokana na amani na utulivu endelevu uliopo nchini.

# SERA YA MAMBO YA NJE YENYE TIJA



**Hali halisi:**

- Tanzania imepoteza ujasiri na uongozi uliokua nao ulimwenguni kwenye Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya SADC.

- Vilevile mikwaruzano na majirani zetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Malawi kumepelekea kuzorota kwa mahusiano yaliyokuwepo kihistoria.

**Fursa:**

- Historia yetu inatubeba katika medani ya kimataifa kwa mfano uamuzi wa kutishia kujitoa kwenye Jumuiya ya Madola endapo Afrika Kusini ingepewa uanachama ni mojawapo ya mambo ambayo yaliifanya Tanzania (Tanganyika wakati huo) itiliwe maanani na majirani zetu, Afrika na hata mataifa makubwa ya dunia.

- Umoja wetu wa Kitaifa, ukizingatia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.
- Hazina kubwa ya maliasili kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na ongezeko kubwa la mahusiano ya kiuchumi na biashara hasa kupitia uwekezaji katika madini, mafuta na gesi.
- Hazina ya historia kubwa ya utamaduni na ustaarabu duniani.



**CHADEMA itafanya nini:**

- Kukuza ushirikiano wa Kimataifa wenye tija na Ujirani mwema.
- Kutetea haki za binadamu, usawa wa nchi na kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika diplomasia ya kimataifa.
- Kukuza umoja na ushirikiano wa Afrika ndani ya AU, EAC na SADC.

- Kuimarisha Umoja wa Mataifa ikiwa ni pamoja na kudai mabadiliko ya mfumo ili kuleta usawa wa nchi shiriki.
- Kujenga uwezo na ujuzi wa kuingia mikataba yenye tija ya uwekezaji wa kimataifa ikiwemo mikataba ya kubadilishana madini nakadhalika kwa teknolojia na viwanda.

**Matokeo tarajiwa:**

- Inatia mkazo katika kujitegemea na kuifanya Tanzania isiwe ombaomba.
- Inakuza diplomasia ya uchumi na maendeleo.
- Inatetea wanyonge popote pale duniani.
- Inaiunganisha Africa na Waafrika.


‘MALIASILI ZETU KWA MAENDELEO YETU’




# Time for Change